



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA UMMA**

**MAAMUZI YA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA KUHUSIANA NA  
KESI YA KIKATIBA ILIYOFUNGULIWA NA BWANA PETER  
KIBATALA DHIDI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI NA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI (NEC)**

Kufuatia maamuzi yaliyotolewa na Mahakama Kuu ya Tanzania leo tarehe 23 Oktoba 2015 Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kuwafahamisha wananchi wote hasa Wapiga Kura kuwa;

Mahakama kuu imetoa tafsiri ya kifungu cha 104(1) cha sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, kinachosema nanukuu "***Hakuna mtu yeyote atakayefanya Mkutano siku ya kupiga kura au; ndani ya jengo lolote ambamo upigaji kura katika Uchaguzi unaendelea, au kuonyesha kadi ya picha yoyote, upendeleo au nembo nyingine inayoonesha kuunga mkono mgombea fulani katika Uchaguzi'***" mwisho wa kunukuu.

**Kuwa ni kifungu halali K ikatiba.**

Kutokana na tafsiri hiyo Mahakama Kuu imeamua yafuatayo:-

- 1. Hakuna mtu yeyote atakayeruhusiwa kukaa umbali wa mita 200 kutoka kituo cha Kupigia Kura.**

**2. Hakuna kusanyiko lolote litakaloruhusiwa siku ya kupiga kura.**

**3. Hakuna kuvaa sare ya Chama, kuonesha Nembo au upendeleo kwa Mgombea yeyote au Chama chochote.**

**Aidha, Mahakama imetamka rasmi kuwa maelekezo yaliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi chini ya vifungu vya 104 (1) na 126 vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 103 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 na vipengele 2.2 (j) na 2.3 (c) (e) vya Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2015, ambavyo vinamzuia mtu yeyote kukaa umbali wa mita 200 bila sababu ya msingi katika vituo vya kupigia, kuhesabu na kujumlishia kura yaendeleo kuheshimiwa.**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inasisitiza kuwa wananchi wanatakiwa kufuata maelekezo yanayotolewa na Tume ikiwa ni pamoja na kuheshimu Sheria na taratibu zote za Uchaguzi.

Kailima, R. K

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**